BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI, KUHUSU UTEKELEZAJIWA MAAGIZO YA KAMATI YA MWAKA 2021/2022 KWA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

**Mheshimiwa Spika,** nianze hotuba hii kwa kumshukuru sana Mola wetu Mtukufu kwa kuendelea kutujalia uzima na afya njema. Aidha nimshukuru sana Muumba kwa jinsi anavyoendelea kuijalia nchi yetu kuwa ya amani na utulivu na kutuwezesha kukutana tena katika mkutano huu ili kujadili namna ya kuharakisha maendeleo ya Taifa letu. Vilevile, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutekeleza kazi zetu za Uwakilishi kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Pia napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kutuongoza vyema na kwa uweledi mkubwa kwenye Baraza hili Tukufu na kunipa nafasi ya kusimama na kuwasilisha hutuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile napenda kuushukuru uongozi mzima wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa ushirikiano wanayoipa

kamati yetu wakati wa kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa maelekezo ya Kanuni ya 109, fasili ya 18 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020, naomba kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba, Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi imepitia Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yetu ya Mwaka 2021/2022 kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi na kuridhika kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Maagizo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kwa dhati kabisa inaipongeza Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kupitia taasisi zake zote kwa kuongeza ufanisi unaotokana na kutafuta watendakazi wataalamu, vitendea kazi pamoja na kuongozewa bajeti kwa mwaka huu wa fedha. Kamati inaamini kwamba, hatua hii itaongeza kasi ya utendaji na kutekeleza majukumu yao kitaalamu na kwa ufanisi zaidi. Kamati inazidi kuiomba Serikali kuhakikisha fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Wizara hii zipatikane kama zilivyoombwa na kwa wakati uliokusudiwa ili kuweza kufanikisha malengo na shabaha zilizowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusiana na masuala ya Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC), Kamati yangu inaunga mkono uwamuzi wa Wizara kupitia Shirika

hilo wa kutenga Jumla ya Shilingi Bilioni 16 kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo nyumba za Maendeleo zikiwemo nyumba za Serikali. Kwa upande mwengine Kamati inahimiza kuendelezwa kwa mazungumzo na wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza katika ujenzi wa nyumba za wananchi pamoja na watumishi wa Serikali. Tunaamini kwamba, jambo hili likifanikiwa litasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la ukosefu wa makaazi kwa watumishi na wananchi wetu na pia kwenda sambamba na nia ya serikali ya Awamu ya nane ya kuendelea kutoa huduma bora za maisha kwa wananchi wote.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na habari hizo njema kwa Shirika letu la Nyumba, Bado Kamati yangu inasisitiza kuheshimiwa na kufuatwa kwa Sheria, na taratibu zote zinazofaa kufuatwa kwa wapangaji wote wa nyumba za Serikali. Hapa Kamati yangu inazidi kutoa angalizo hasa kwa sisi viongozi tuliopewa dhamana tutimize wajibu wetu na tuhakikishe tunawashajihisha wananchi wetu waliopanga katika nyumba hizo kufuata mikataba yote waliyokubaliana na Shirika ama serikali kwa ujumla ili kuhakikisha mpangaji na mpangishaji kila mmoja anatimiza wajibu wake ili hatimae kuepusha migogoro inayoweza kutokea iwapo mikataba hiyo itakiukwa.

**Mheshimiwa Spika,** Nikigusia katika Sekta ya Ardhi, Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati inakubaliana na uwamuzi wa Wizara wa kuelimisha kuanzia Wilaya hadi Shehia pamoja na wananchi ikiwa ni njia moja wapo ya kupunguza changamoto za migogoro ya ardhi katika jamii. Aidha Kamati inaunga mkono mashirikiano ya kisekta yanayoendelea kuchukuliwa hasa katika Taasisi zetu za Mahakama ya Ardhi na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha umakini unakuwepo hasa katika haki ya matumizi ya ardhi kusudi ili kujikinga na migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi.

Aidha Kamati yangu kupitia fursa hii, inaendelea kuelezea masikitiko yake kutokana na tatizo la ukosefu wa Mipango Miji na Vijiji katika Manispaa zetu. Tunaendelea kuzihimiza taasisi zinazohusika na mipango hii kutimiza wajibu wake ili kujikinga na migogoro na usumbufu  wa kila siku katika makaazi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kupitia ripoti yetu ya Kamati tuliyoitowa mwezi wa Februari mwaka huu kwa Wizara ya Ardhi na Maandeleo ya Makaazi, pia tuligusia suala kuchukuliwa hatua za upimaji wa maeneo ya serikali na kupatiwa Hati miliki ili kuepusha uvamizi. Majibu ya utekelezaji wa Wizara yanaonesha kwamba Wizara ya Maendeleo ya Ardhi na Makaazi iko tayari kufanya shughuli hiyo, na inaziomba taasisi zote kuanisha maeneo wanayotaka kupimiwa ili wizara iweze kuchukua hatua.

Hata hivyo, hadi Kamati inapokea taarifa ya utekelezaji wa Agizo hilo jumla ya Wizara saba tu, ndizo ambazo zilizowasilisha orodha ya maeneo yao na tayari yameanza

kufanyiwa kazi. Hivyo Kamati inazisisitiza Taasisi zilizobaki kuharakisha kuwasilisha maeneo yao ili yatambuliwe na kupimwa na baadae baada ya kukamilisha malipo zipatiwe hati miliki za maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile kamati imefarajika baada ya kupokea taarifa kuwa jukumu la malipo ya fedha za kupatiwa hati kwa Wizara na Taasisi za Serikali kwa sasa litakuwa chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, hivyo basi, kamati inazisisitiza Wizara na Taasisi zote zilizokuwa bado hazijakamilisha kufanya maombi ya hatimiliki za maeneo na majengo basi zifanye haraka kukamilisha maombi hayo ili kuepusha changamoto za uvamizi kwa mali za Sekali.

**Mheshimiwa Spika,** Namalizia hotuba yangu kwa kugusia maagizo yanayohusu Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA), Kamati inashauri kwamba Wakala utumike kama ilivyo dhamira iliyokusudiwa wakati wa uundwaji wake. Hapa tunatoa wito kwa Wajenzi wote hasa katika majengo ya Serikali kuitumia ZBA katika hatua za awali za Miradi ya Ujenzi badala ya kuwatumia kwa kuomba ushauri pale miradi hiyo inapokubwa na hitilafu za kiujenzi na utetekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa naomba kuchukua fursa hii kwa kuwashukuru kwa dhati Kabisa Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mashirikiano yao waliyonipa wakati tukipitia utekelezaji wa maagizo haya, na kwa ruhusa yako naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Yahya Rashid Abdulla(Mamba) - Mwenyekiti
2. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir - Makamo Mwenyekiti

3. Mhe. Bakhati Khamis Kombo - Mjumbe

4. Mhe. Mussa Foum Mussa - Mjumbe

5. Mhe. Kombo Mwimyi Shehe - Mjumbe

6. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe

7. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu

8. Ndg. Himid Haji Choko - Katibu

**Mheshimiwa Spika,** Nimalizie kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza kwa umakini na kwa utulivu mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

**……………………**

**(Mhe.Yahya Rashid Abdulla -Mamba)**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**